**LEARNING BY EAR**

**“Mihadarati na vileo – Poromoko la jamii”**

**Episode 8: “Pekua, kisha fichua”**

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo**

**PROOFREADER: Charlotte Collins**

**List of characters by scene:**

**<u>SCENE ONE: CHUNGA SANA, ON A STREET CORNER</u>**

- **Bamju (m, 40)**
- **Okosho (m, 18)**

**<u>SCENE TWO: AT THE LOCAL PRESS OFFICE</u>**

- **Beri (f, 45)**
- **Mugo (m, 40)**

**<u>SCENE THREE: OKOSHO'S ROOM</u>**

- **Zula (m, 18)**
- **Jabali (m, 18)**

**<u>SCENE FOUR: OUTSIDE BERI'S HOME</u>**

- **Beri (f, 45)**

- **Waziri Kafegi (m, 55)**
- **Inspekta Tino (m, 40)**

## SCENE FIVE: AT CHUNGA SANA BUS STOP

- **Zula (m, 18)**
- **Jabali (m, 18)**

**MSIMULIZI (m/f)**

**INTRO:**

Salaam tele na karibu katika kipindi cha Noa bongo! Jenga maisha yako**.** Tuko katika kipindi cha nane katika tamthilia hii kwa jina **“Poromoko la jamii”.** Katika kipindi kilichopita, Jabali alimuokoa Zula kutoka kwa umati ulotaka kumua. Kamishna Beri akapokea simu kutoka kwa waziri Kafegi kumjulisha kuwa amepewa uhamisho wa lazima. Hadithi hii itatufikisha wapi? Kaa nasi ujue yote, kwani leo kipindi chaitwa **“Pekua, kisha fichua”.** Tunaanzia pale barabarani kwenye umati mkubwa baada ya Jabali kuwashawishi wampe nafasi nyingine Zula. Lakini Zula hakua pekee yake walipombakura kibeti aliyekuwa mwalimu mkuu wao wa zamani, Bi. Chacha. Okosho ndiye aliyenyakua kibeti hicho pamoja na pesa zilizokuwa ndani, hivi sasa alikuwa akikutana na Bamju kununua heroini.

**SCENE ONE: CHUNGA SANA, ON A STREET CORNER**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | **SFX: LIGHT TRAFFIC AND HOOTING FROM A DISTANCE** | |
| 2. | **OKOSHO:** | **(shocked)** Ati! 500? Hapana, Bamju! Si ilikuwa ni 250. |
| 3. | **BAMJU:** | Mambo yamebadilika. Mahitaji yamezidi. |
| 4. | **OKOSHO:** | **(cursing, aside)** Sawa, kama ningelijuwa. Zula na mimi tungekuwa twaendesha magari sasa. Sawa. Nipe kifurushi kimoja. Pesa yako ndio hii. |
| 5. | **SFX: HANDBAG WITH ZIPPER BEING OPENED** | |

6. **BAMJU:** Sina masalio. Kwanini usichukuwe mbili kwa elfu moja?

7. **OKOSHO:** Hata wacha mbili, nipe vinne. Nina elfu mbili.

8. **BAMJU:** Lahaula! Sawa. Ulipata wapi pesa zote hizi, Okosho? Eh? Na utumie taratibu, usipapie, hii mali ni kali, si unajuwa, muna “party” kwani?

9. **OKOSHO:** La, hii ni yangu na Zula; kama bado yuko hai basi.

10. **BAMJU:** Eti nini?

11. **OKOSHO:** Usijali. Nipe mali yangu niondoke.

12. **MSIMULIZI:** Ni suala la kuchujua moyo unapoona athari za mihadarati kwa watumizi wake. Mbali na kuwadororesha afya zao, mihadarati huwafanya wakaishi katika maisha ya ndoto. Wao hujali tu, atafanyaje apate kileo chake tena. Okosho amefikia kilele hicho sasa. Ataelekea wapi? Tukimeza mate, kamishna wa polisi Beri, baada ya kupata simu ya Waziri Kafegi, haraka aliketi chini na akaandika arafa haraka, akaondoa kila kilicho chake dawatini kwake na kuiacha barua hiyo hapo juu ya meza. Lakini atatorokea wapi?, Beri aliweka tumaini lake mahala pamoja tu.

**SCENE TWO: BERI AT THE LOCAL PRESS OFFICE**

13. **SFX: BUSY WORKING OFFICE AMBIENCE**

14. **MUGO:** Hujambo. Mimi ni Bw. Mugo, mhariri mkuu wa gazeti la “The Voice”. Tafadhali nifuate afisini mwangu.

15. **SFX: DOOR OPENED THEN CLOSED**

16. **MUGO:** Karibu kiti. Kuna tatizo iwapo nitavuta sigara?

17. **BERI:** Ndio! Bw. Mugo, una kibandiko hapo nje ya afisi yako kinachosema uvutaji sigara hauruhusiwi afisini.

18. **MUGO:** Ni kweli, hiyo ni sheria ya kampuni. Lakini mara moja moja,si unajuwa, kupunguza uzito wa kazi, na kupumzika kidogo tuna…

19. **BERI:** Hayo ndiyo mambo yaliyotufikisha hapa tulipo hii leo. Kweli utachukuwa muda kunisikiliza hadithi yangu?

20. **MUGO:** Bila shaka, bila shaka. Nina hamu sana ya kuisikia. Lakini kabla tuanze, nieleze kama una ushahidi wa kutosha kuwa watu maarufu nchini wanahusika na sakata hii ya mihadarati, ni kwanini usiwashike na uache mahakama iwaamulie hatima yao?

21. **BERI:** Baada ya yote niliyopitia… siamini tena mtu yeyote..

**22.** **MUGO:** Je, mimi? Si unajuwa vyema hawa wabunge wana hisa fulani katika kampuni hii yetu ya kutoa habari.

**23.** **BERI:** Nafahamu. Lakini nakumbuka ukiwa mwanahabari chipukizi uliongoza maandamano ya kudai haki za wanahabari. Mimi pia naunga mkono haki hizo.

**24.** **MUGO:** **(thoughtful)** Nafurahi kusikia hivyo. Naam… kweli hizo zilikuwa nyakati ngumu.. ngoja kidogo...

**25.** **SFX: PAGE FLIPPED AND PEN SCRIBBLING ON PAPER (studio)**

**26.** **MUGO:** Ukiwa tayari nami niko tayari...

**27.** **MSIMULIZI:** Beri alimueleza Mugo kinaga ubaga, ima fa ima, akampa ushahidi wote wa uchunguzi wake. Mugo akiandika kurasa baada ya nyingine, aliacha kuandika wakati tu alipotaka kufafanuliwa zaidi au kuelezwa kwa undani zaidi maswala fulani. Wakati Beri akifichua yote, katika barabara kuu ya Chunga Sana, Jabali alimpeleka Zula katika kliniki ya mtaani ili apate matibabu ya majeraha aliyopata kutokana na kupigwa kwake, Zula akapewa ruhusa kurudi nyumbani na yeye pamoja na Jabali wakaanza kumtafuta Okosho wamuulize kuhusu kibeti cha Bi. Chacha.

**SCENE THREE: OKOSHO'S ROOM**

28. **SFX: NOISE OF A BUSY STREET IN THE BACKGROUND**

29. **JABALI:** Zula, una hakika hii ndio nyumba muliopangisha?

30. **ZULA:** Ndio. Hapa ndio maskani. Sipasahau kwa sababu ya huu mti wa bangi nilioupanda.

31. **JABALI:** **(shocked)** Mungu wangu! Kweli ni mti wa bangi. Ulifikiria nini, Zula? Unajuwa unaweza kuingia shidani ukionekana na polisi? **(sighs deeply)** haidhuru tutatue hayo baadaye, kwanza.. wacha tuone kama Okosho yuko…

32. **SFX: SEVERAL KNOCKS ON DOOR**

33. **ZULA:** Yuko. Labda awe amekolewa na ulevi.

34. **JABALI:** Kwani ni mlevi tayari? Lo! Kwani muligeuka lini mukawa hivi? Sawa, itabidi tuingie kwa nguvu. Hatuwezi kusubiri.

35. **SFX: DOOR PUSHED OPEN BY FORCE**

**36. JABALI:** **(disgusted)** Fyuuu! Harufu gani hii jamani? Puuuu…na mbona kuna giza namna hii? Mwaishi vipi humu? Mulipeza lini kufagia mwisho? Wewe mwenyewe mwisho ulioga lini? Humu ni kuchafu hata kombamwiko yaani mende wenyewe watawaomba kandambili.

**37. ZULA:** Sikumbuki. Kila tukija huwa tuko ndii.

**38. JABALI:** Ati?... **(calls out)** Okosho, uko wapi? Ni Jabali na Zula. **(pause)** Labda hayuko.

**39. ZULA:** Si huyu hapa. Huyu kitandani.

**40. JABALI:** Muna kitanda humu? Kiwapi? Oh, nakiona sasa…Mungu wangu! **(in panic)** Okosho! Okosho! Amka!

**41. ZULA:** **(trembling voice)** Hapana… hapana… yani amejidunga nne!

**42. JABALI:** Nne? Nini nne?

**43. ZULA:** **(almost breaking down in tears)** Kuna paketi tupu nne za heroini. Kawaida moja tu inatutosha wote wawili kutumia. Nafikiri Okosho amezidisha kiwango. Mtazame, ashaaga dunia.

**44. JABALI:** **(confused and shocked)** Amekufa? La! Ati heroini? Zula, unasemaje?

**45. ZULA:** Tumechelewa. Amefariki, Jabali. Rafiki yetu Okosho ametuaga. **(now weeping)**

***46.*** **JABALI:** **(also breaking down in tears)** Okosho…! Huwezi kuaga bila kwaheri . amka !... *haiwezekani!!!!!!!!!!*

**47. MSIMULIZI:** Jabali akaita polisi na wahudumu wa dharura, ambao walibainisha kifo cha Okosho kilichotokana na matumizi ya heroini yaliyozidi kiwango mwilini. Haya hutokea kwa watumizi wasipojuwa wanatumia nini. Aghlabu huwazidi nguvu; au wauzaji wanapo baka kemikali hizi kwa kuziongezea kemikali nyengine kama vitoa rangi. Hii ndiyo sababu kuu ya watumizi kupata majeraha ya kudumu, kama upofu, baada ya kunywa mikorogo hii. Siku baada ya tanzia ya Okosho, magazeti yalienea vichwa tetesi kama: “Magwiji ya serikali ndio huleta mihadarati” - “ Viongozi ndio vinyozi mihadaratini” – “ Je, vita vya madawa ya kulevya vimetushinda?” Beri akinunuwa nakala yake alishtuliwa na mlio wa simu yake.

**SCENE FOUR: OUTSIDE BERI'S HOME**

48. **SFX: MOBILE PHONE RINGING**

| | | |
|---|---|---|
| **49.** | **BERI:** | **(answers call)** Habari ya asubuhi, Beri anaongea. Ni nani mwenzangu? |
| **50.** | **MHE. KAFEGI:** | **(furious, threatening)** Nani mwenzako? Ni waziri Kafegi! Haya ndiyo malipo yako? Hii ndio shukurani yako kwa serikali? |
| **51.** | **BERI:** | Sikuwa na budi, Waziri. Nimejiuzulu. Lakini najivunia nilichofanya. Kama huna hatia basi huna haja ya kuwa na wasiwasi. Sina ubinafsi; napigania wasichana na wavulana ambao maisha yao yamezambaratika kwa ajili ya mihadarati. |
| **52.** | **MHE. KAFEGI:** | Nimetumikia nchi hii miaka mingi kuleta usalama na kumaliza uhaini. Hata kuna uchunguzi nilioanzisha kuhusu biashara za mihadarati na vileo. Kwanini hukuelezea chochote kuhusu hayo? |
| **53.** | **BERI:** | Waziri Kafegi, hiyo ni kejeli, mwizi anawezaje kujishika mwenyewe? Kama askari polisi; najua uchunguzi wako ni kifumba macho watu kuonekane kuna kitu kinaendelea. Ni miaka mingapi tangu uanze upelelezi? Miwili? Mitatu? **(Silence)** |

**54. MHE. KAFEGI:** Sikiliza. Ikinilazimu kujiuzulu kwa ajili ya hii kesi.. au kama… nitahusishwa kortini, naapa kwa kaburi la mamangu… utajuta siku uliyozaliwa!!!

**55. BERI:** Vitisho vyako vimechelewa, Waziri. Kila kitu ki parwanja peupe. Kimechapishwa kwenye magazeti, kwenye mitandao, kwenye tovuti na kwengineko…bila shaka unajuwa hiyo inamaanisha nini? Ulimwengu mzima unatazama kesi hii.

**56. MHE. KAFEGI:** Na mimi ninakutazama wewe!

**57. SFX: MOBILE PHONE CALL DISCONNECTED WITH BEEPING SOUND**

**58. BERI:** Jamani! Mbona nimejitia kwenye hili vurugu? Ah – acha nijue Tino anaendeleaje….

**59. SFX: MOBILE PHONE NUMBER BEING DIALLED**

**60. BERI:** Habari ya asubui, Tino. Unaonaje maisha ya nje ya kikosi cha polisi?

**61. INSP. TINO:** Magumu mno. Natamani kuwa kazini, niliapa lazima nimueke Bamju korokoroni. Lakini ulipojiuzulu, sikuwa na budi ila kufuata nyayo zako.

**62. BERI:** Unajuwa, bado unaweza kurudi kazini. Hata hivyo, umesoma gazeti la leo?

**63. INSP. TINO:** La, kwanini? Kumetokea nini? Afrika inapeleka mtu wa kwanza mwezini?

**64. BERI:** **(laughs)** La... mazuri kuliko hayo! Nenda ujipatie nakala.

**65. MSIMULIZI:** Kwa mara ya kwanza baada ya majuma mengi, Beri alicheka na kutaniana na mwenzake, Tino. Lakini vitisho vya waziri Kafegi kweli vitakuwa? Tuendelee kusikiza… Jabali ana mambo kemkem ya kumuarifu Chambo asubui hii. Alimshawishi Zula waende naye afisini kwao katika, kituo cha basi cha Chunga Sana. Lakini walipofika pale...

**SCENE FIVE: AT CHUNGA SANA BUS STOP**

**66. SFX: BUSES AND VAN ENGINES REVVING**

**67. JABALI:** Siamini kuwa Okosho sasa ni marehemu. Tena kifo cha uchungu kweli kweli.

**68. ZULA:** Lau sio wewe, hata mimi ningelikuwa marehemu. Nakushukuru kuniokowa. Sijui nitakulipa nini au vipi.

**69. JABALI:** La, Zula. Sisi ni marafiki. Marafiki ni wa wakati wowote. Chambo akija atakueleza jinsi ya kukata hamu na kuacha mihadarati. Sijui amechelewa wapi. Siyo kawaida yake.

**70. ZULA:** Labda ametekwa nyara. Hawa watu wa hii biashara si wema, Jabali. Kuua kwao sio kitu.

**71. JABALI:** **(worried)** Jamani! Yaweza kuwa ni kweli, Zula. Chambo amejitolea muhanga kupigana na utumizi wa mihadarati.

**OUTRO**

Jabali aliingiwa na uoga wa ghafla kwa wazo hili ya kwamba Chambo labda katekwa nyara na wahalifu wa mihadarati na hata kuuliwa. Lakini ni kweli hayo? Ni nini kilichomtokea Chambo? Na Zula atakubali kuenda kwenye jumba la kurebisha tabia waathiriwa mihadarati? Huu ndio mwisho wa Beri na Tino? Mheshimiwa Kizito yuko ng’ambo, je atapokelewa vipi akirudi? Kwa haya na mengine… jiunge nasi wiki ijayo. Pia tembelea tovuti yetu www.dw.de/lbe. Hadi wakati mwengine, kwaheri kwa sasa.